

Tathmini ya Matumizi ya Istilahi za Kitehama kwa Wazungumzaji wa Kiswahili: Mifano Kutoka kwa Watumiaji wa Simu nchini Tanzania

Majura Nyangaywa¹ na Pendo S. Malangwa²

¹Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

²Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Makala haya yanaangazia hali ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za kitehama za Kiswahili za simu za mkononi mionganoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili nchini Tanzania. Data za uwandani zilikusanya kutoka kwa watoa taarifa 68 katika kata za Kimara na Ubungo, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Tanzania. Data zilikusanya kwa mbinu ya usomaji wa matini, hojaji na usaili. Nadharia ya Ulingenifu wa Kiathari ilitumika kuongoza utafiti huu. Matokeo ya utafiti yamechambuliwa kwa mkabala wa kitaamuli na kitakwimu. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, upokelewaji wa istilahi za Kiswahili za programu za simu za mkononi, una mambo mchanganyiko mionganoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili. Baadhi ya istilahi zinakubaliwa na nyingine ama hawazielewi au hawazikubali. Wanaikubali istilahi hizo, wanatoa sababu mbalimbili zikiwemo urahisi na uelewekaji wa istilahi za Kiswahili. Sababu nyingine ni ugumu wa istilahi za Kiingereza zilizopo katika programu za simu. Kwa upande mwingine, sababu zinazowafanya baadhi ya watumiaji wa simu kutozikubali istilahi za Kiswahili wanaona kuwa, ni ushamba kutumia Kiswahili kwenye simu iliyowekewa Kiingereza tayari. Pia, wanaiona lugha ya Kiingereza kuwa ni lugha ya Kimataifa. Hivyo, makala haya yanapendekeza kwamba, kuna haja ya kutathmini michakato ya uundaji wa istilahi za programu za simu, kuwashirikisha watumiaji wa simu wanaozungumza Kiswahili ili kuunda istilahi kubalifu.

Maneno Muhimu: Tathmini, Matumizi, TEHEMA, Istilahi

Utangulizi

Simu za mkononi ni matokeo ya uvumbuzi uliofungamanisha sayansi na teknolojia. Simu za mkononi, ambazo ni mionganoni mwa vifaa vya teknolojia ya mawasiliano, huja na programu zenye istilahi za lugha chanzi kama vile Kifini (Nokia), Kichina (Tecno) na Kiingereza (Apple) zilizobuniwa awali na watengenezaji wa simu zinazohusika (Okyere na wenzie, 2016). Kamau (2007) anaeleza kuwa, usambazaji na utumiaji wa teknolojia ya mawasiliano, zikiwemo kompyuta na simu, hutegemea lugha. Nchi nyingi za Kiafrika, huipokea teknolojia hii kwa lugha za kigeni. Kamau anafafanua zaidi kuwa, watumiaji wengi walolengwa kuitumia teknolojia hii katika bara la Afrika, hawawezi kuzitumia istilahi hizi kwa kuwa, baadhi yao hawazielewi zikiwa katika lugha chanzi. Katika hali kama hii, kunatokea haja ya kuhawilisha istilahi za teknolojia ya mawasiliano kwa kuzijanibisha katika lugha za Kiafrika ili ziweze kutumiwa na walengwa wa vifaa vya mawasilaino vinavyohitajika. Akishadidia jambo hili, Sanday (2014) anaeleza kuwa, ujanibishaji wa lugha za kigeni katika lugha za Kiafrika kuititia teknolojia ya mawasiliano, unawezesha kuondoa vikwazo vya lugha kwa wasioelewa vema lugha za kigeni.

Kutokana na umuhimu wa ujanibishaji, baadhi ya kampuni za teknolojia ya mawasiliano, zikiwamo Linux na Microsoft, zimeanza kujanibisha teknolojia zao kwa lugha lengwa za Kiafrika ambapo Kiswahili ni mionganoni mwa lugha za awali zilizonufaika na ujanibishaji huu. Kwa kawaida, shughuli ya ujanibishaji hufanywa na wataalamu wa uundaji wa istilahi. Jitihada hizo za ujanibishaji hujumuisha kutafsiri au kuunda istilahi za teknolojia ya mawasiliano kwa lugha mbalimbali.

Kwa mujibu wa wataalamu, shughuli ya kuunda istilahi za uga wowote hulenga kuunda istilahi zinazozingatia sifa mahususi. Felber (1984) anaeleza sifa za istilahi sadifu kuwa ni: usahihi, ufupi,

urahisi wa kutamkika na kuandika, urahisi wa kunyambuka, uzingativu wa sarufi ya lugha lengwa, uwakilishi wa dhana moja tu na udhana. Aidha, Tumbo-Masabo na Mwansoko (2008) wanapendekeza misingi mahsusini inayopaswa kuzingatiwa katika uundaji wa istilahi. Misingi hiyo ni pamoja na: istilahi kuakisi sifa bainifu za dhana zinazowakilishwa, istilahi kuweza kunyambulika ili kuwezesha kuundwa kwa istilahi zingine za kikoa hichohicho, istilahi zenyenye vivuli vya maana zinazoingiliana kuwa na ulinganifu wa mtiririko, istilahi kuwa na utoshelevu na ufupi ili kuziwezesha kueleweka kirahisi, istilahi mahuluti na finyazo kuepukwa na kila istilahi kuwakilishwa na dhana moja tu. Kwa misingi hiyo, inatarajiwaa kwamba istilahi za teknolojia ya mawasiliano zinapoundwa zikidhi haja hiyo. Hata hivyo, licha ya istilahi za kitehama za Kiswahili kuendelea kuundwa na kutumiwa na baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili, bado haijajulikana kwa yakini watumiaji lengwa wanazipokeaje na wanazikubali kwa kiasi gani.

Malangwa (2010) anafafanua kuwa mkanganyiko wa istilahi za kiufundi zinazoundwa au kutafsiriwa, unasababishwa na ushirikiano hafifu mionganini mwa wataalamu wa lugha. Wataalamu hawa hujumuisha, walimu wafundishao lugha, wanateminografia, wanaleksikografia. Malangwa anaongeza kuwa, sababu nyingine ya mkanganyiko wa istilahi za kitehama ni mbinu tenge zinazotumiwa katika tafsiri ambapo hutokeza istilahi moja katika lugha chanzi kuwa na visawe zaidi ya kimoja katika lugha lengwa. Akishadidia jambo hili, Kinyanjui (2014) anatolea mifano ya istilahi zilizoundiwa visawe zaidi ya kimoja ikiwamo, istilahi ‘monitor’ ina visawe zaidi ya kimoja ambavyo ni; monita, kiwaa, kiwambo na mulishi. Istilahi nyingine ni ‘Setting’ yenye visawe zaidi ya kimoja ambavyo ni; kipimo, mpangilio, mpangizo. Kadhalika, istilahi ‘recyclebin’ ina visawe zaidi ya kimoja ambavyo ni; kisaduru, kijalala na urejelezaji.

Kuwepo kwa visawe zaidi ya kimoja, vikiwakilisha istilahi moja katika lugha chanzi huchukuliwa kuwa mkanganyiko wa istilahi za kitehama unaojitokeza kwa wazungumzaji. Katika hali kama hiyo, watumiaji wa lugha lengwa wanashindwa kujua ni istilahi ipi itumiwe katika mazungumzo yao ya kila siku wanaporejelea dhana mahsusini. Kwa kuzingatia msingi huo, makala haya yanaangazia tathmini ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za Kitehama kwa wazungumzaji wa Kiswahili watumiao simu za mikononi nchini Tanzania.

Nadharia

Utafiti wetu ulitumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kiathari ni nadharia ya tafsiri ya kimawasiliano iliyosisiwa na Nida miaka ya 1960 na kusasishwa na Nida na Taber (1969). Mhimili wa Nadharia hii unabainisha kuwa, tafsiri sharti ilete maana sawa kwa hadhira ya lugha lengwa kama ilivyokuwa kwa hadhira ya lugha chanzi katika muktadha asilia. Mkazo wa nadharia hii ni kuwa ujumbe sharti urekebishwe kutokana na mahitaji ya kiisumu, mategemeo na malengo ya hadhira katika uhalisia. Mfasiri (ambaye katika muktadha wa makala haya ni muundaji wa istilahi za kitehama) atafute visawe (istilahi za kitehama za Kiswahili) vya karibu zaidi na ujumbe wa lugha chanzi ili kuwezesha hadhira lengwa (ambayo katika makala haya ni wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mikononi) kufahamu maana za visawe (yaani istilahi za kitehama) za programu za simu za mikononi. Nadharia hii ilimwongoza mtafiti katika kupambanua hali ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za Kiswahili za kitehama mionganini mwa wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mikononi.


Methodolojia ya Utafiti

Methodolojia ya utafiti huu ilijumuisha mbinu za usampulishaji na ukusanyaji wa data pamoja na uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo. Katika sehemu hii tutaeleza kwa kifupi mbinu hizi na jinsi tulivyozitumia. Mbinu ya usampulishaji sahili ilitumika kupata watumiaji 68 wa simu wanaozungumza Kiswahili. Eneo lililotumika kupata data ni Kata za Kimara na Ubungo, manispaa ya Ubungo, nchini Tanzania. Mchakato wa kuwapata watumiaji wa simu ulizingatia utayari wao, utumizi wa simu za mikononi na ujuzi wa kusoma na kuandika Kiswahili. Data zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji wa matini, hojaji na usaili. Mbinu ya usomaji matini ilitumika kukusanya istilahi za programu za simu. Simu zilizotumika ni za aina ya Nokia, Itel na Tecno. Kupitia mbinu hii tulipata istilahi za simu kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kisha kuzipanga kwa mpangilio wa alfabeti. Aidha, mbinu ya hojaji ilitumika kukusanya data kwa watumiaji wa simu 68 waliozijaza na kuzirejesha.

Hojaji hizi zilihusu matumizi ya istilahi na mtazamo wa wazungumzaji kuhusu kutumia au kutotumia istilahi za Kiswahili za programu za simu. Usaili ulihusu watumiaji wa simu kubainisha sababu zinazowafanya watumie au wasitumie istilahi za Kiswahili za simu katika simu. Data zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa mkabala wa kitaamuli na kitakwimu.

Hali ya Matumizi na Kukubalika kwa Istilahi za Kitehama

Suala la matumizi ya istilahi za kitehama kwa watumiaji wa simu limechukuliwa kimuktadha katika makala yetu. Katika makala haya, tunarejelea idadi ya watumiaji wa simu wanaotumia au wasiotumia istilahi za Kiswahili za kitehama katika simu za mkononi. Hivyo, usafanuzi umetolewa kitakwimu ili kuonyesha hali ilivyo ya wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia istilahi za Kiswahili za programu za simu za mkononi. Ili kujua matumizi ya istilahi hizi, watoa taarifa 68 waliulizwa swali lilikuwa linasema “simu yako ya mkononi unaitumia ikiwa katika lugha gani?” Lengo la swali hili lilikuwa kufahamu ni lugha ipi hasa inatumiwa na wengi kati ya Kiswahili, Kiingereza au lugha nyinginezo katika programu za simu. Lugha hizi kama zilivyowekwa katika hojaji, zilikusudiwa kudhihirisha hali ya matumizi ya istilahi za kitehama, kwa wazungumzaji wa Kiswahili ambao ni watoataarifa. Matokeo yanaonesha kuwa jumla ya watoataarifa 68 walijibu swali hili. Mto taarifa mmoja, 1 alisema anatumia lugha nyingine tofauti na Kiswahili na Kiingereza, Watoataarifa 5 walisema wanatumia istilahi za kitehama za Kiswahili. Watoataarifa 62 walisema wanatumia istilahi za kitehama za Kiingereza. Uwasilishaji zaidi wa asimilia umeonyeshwa katika Kielelezo Na 1.



Kielelezo Na.1: Matumizi ya Istilahi za Kitehama kwa Watumiaji wa Simu

Katika kielelezo Na.1 tunaona hali ya matumizi ya istilahi za kitehama mionganii watumiaji wa simu. Kielelezo Na.1 kinaonyesha mto taarifa mmoja sawa na asilimia 1.4 anatumia simu yake katika lugha nyingine ambayo si Kiingereza wala Kiswahili. Vilevile, watoataarifa 5 sawa na asilimia 7.35 wanatumia istilahi za Kiswahili za kitehama. Aidha, watoataarifa 62 sawa na asilimia 91.17 wanatumia istilahi za Kiingereza za kitehama katika simu zao. Matokeo haya yanatoa sura pana ya hali ya matumizi ya istilahi za Kiswahili za kitehama katika programu za simu za mkononi. Ilitarajiwa kwamba, istilahi za Kiswahili za kitehama, zipokelewe na kutumiwa na wengi mionganii mwa wazungumzaji wa Kiswahili hata hivyo, matokeo ni kinyume chake. Jambo hili lilichochea haja ya kuhitaji kujua zaidi. Katika sehemu inayofuata, zimebainishwa sababu walizozitoa watoataarifa zinazowafanya watumie au wasitumie istilahi za Kiswahili za kitehama za simu.

Sababu za Kutumia Istilahi za Kiswahili katika Simu

Kundi la kwanza la watumiaji wa simu za mkononi lilikuwa na watoataarifa watano. Kundi hili ndilo lilikubali kuwa, linatumia istilahi za Kiswahili za kitehama katika simu. Matokeo yalionyesha kwamba, kundi hili lilikuwa na sababu mbalimbali ambazo zimefanuliwa katika sehemu inayofuata.

Ulewекaji wa Kiswahili kwa Watumiaji

Watoataarifa walidai kuwa, wanatumia istilahi za Kiswahili za kitehama za simu za mkononi kwa kuwa wanaielewa vema lugha ya Kiswahili. Waliongeza kwamba Kiswahili ndiyo lugha pekee inayofahamika zaidi kuliko lugha nyingine nchini Tanzania. Utafiti ulionyesha kuwa Kiswahili ni

lugha ya mawasiliano mapana mionganini mwa jamii ya Watanzania. Tanzania inakadirwa kuwa na lugha za makabila zaidi ya 150 (LOT 2009). Mbali na idadi kubwa ya lugha za makabila haya, watanzania walio wengi wanaunganishwa kwa pamoja kutokana na kuwepo kwa lugha ya Kiswahili. Utafiti ulionyesha kwamba, lugha ya Kiswahili imekwishakita mizizi kwa kipindi kirefu na ndio lugha inayowaunganisha watumiaji wengi wa simu za mkononi wanaozungumza Kiswahili.

Madai ya watoataarifa yanatokana na ukweli kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya taifa la Tanzania. Aidha, ndiyo lugha pekee inayowaunganisha watanzania pamoja na kuwepo kwa makabila mengi. Ndio lugha iliyotumika katika kupigania uhuru. Kiswahili ndiyo lugha iliyopangia kutolea elimu katika shule za msingi na vyuo vya ualimu ngazi ya cheti, hutumiwa katika mikutano, jeshini, bungeni, katika vyombo vya habari, matamasha, makongamano, sherehe na mikusanyiko mingine ya kijamii. Hiryo, ni kweli kwamba lugha ya Kiswahili imekita mizizi zaidi ikilinganishwa na lugha nyingine zilizopo. Ni kwa msingi huo, watoataarifa hawa kuzipatia kipaumbele istilahi za Kiswahili za kitehama katika simu zao si jambo la kushangaza kuliko wangependelea istilahi za lugha nyingine.

Ugumu wa Lugha ya Kiingereza

Watoataarifa walibainisha kwamba, Kiingereza ni lugha ngumu zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Lugha ya Kiswahili imejumuishwa katika kundi la lugha ambishi bainishi (Mgullu 2000). Hii ndiyo sababu, pamoja na sifa nyingine matamshi yake, hutamkwa tofauti na yanavyoandikwa. Hii ni tofauti na lugha ya Kiingereza ambayo maneno yake, hutamkwa tofauti na yanavyoandikwa. Kwa mfano, maneno kama *simu, kitufe, nenosiri* huandikwa na kutamkwa kama yanavyoonekana. Sababu hii ni ya msingi sana linapokuja suala la ugumu wa lugha ya Kiingereza, hii inatokana na ukweli kuwa maneno yanavyoandikwa ni tofauti na yanavyotamkwa. Mathalani, maneno kama *password* aliyezoea kutumia Kiswahili atalazimika kulitamka *pasiwed*. Vilevile, neno *missed calls*, aliyezoea Kiswahili atalazimika kulitamka *misidikolo*. Kutokana na mifano hii, sababu iliyotolewa na watoataarifa ni ya msingi na inafaa kuungwa mkono. Baada ya kuangalia sababu za wazungumzaji kukubali kutumia istilahi za Kiswahili za kitehama za simu, sehemu inayofuata tutaangazia sababu za wazungumzaji kutotumia istilahi za Kiswahili za kitehama.

Sababu za Kutotumia istilahi za Kiswahili za Kitehama katika Simu

Kundi la pili lilitoa sababu za kutotumia istilahi za Kiswahili za kitehama za simu za mkononi. Kundi hili lilikuwa na jumla ya watoataarifa 62 kati ya watoataarifa 68 walioshiriki katika utafiti wetu. Sababu zilizotolewa na kundi hili zilikuwa katika sehemu mbili kimaudhui. Sababu za sehemu ya kwanza zilikuwa na maudhui yenyewe kubeba ragba binafsi walizonazo watoataarifa dhidi ya lugha ya Kiingereza. Sababu za sehemu ya pili zilikuwa na maudhui yenyewe kubeba maarifa finyu walio nayo watoataarifa dhidi ya matumizi ya simu za mikononi. Kimahususi, katika kubainisha sababu hizi, tutaanza na sababu zinazohusu ragba binafsi walizo nazo watoataarifa kuhusu Kiingereza kisha tutamalizia na sababu nyinginezo, zitokanazo na maarifa finyu ya watoataarifa dhidi ya matumizi ya simu za mikononi.

Maneno ya Kiswahili Kwenye Simu ni Tofauti na Yaliyozoleka


Watoataarifa 32 kati ya watoataarifa 62 walidai kuwa, maneno ya Kiswahili yaliyomo katika programu za simu za mkononi ni tofauti na Kiswahili cha kawaida. Waliendelea kufafanua kwamba istilahi za simu za mkononi za Kiswahili ni ngumu kuelewaka kwao. Watoataarifa waliongeza kuwa, maneno yanayotumiwa kwenye programu za simu ni kana kwamba, yanatoka kiwandani au maabara, ambako hakuna jamii ya wasemaji lugha. Baadhi ya istilahi za Kiswahili za kitehama za simu zilizobainishwa na watoataarifa kuwa ni ngumu kuelewaka, zimeonyeshwa katika Jedwali Na 1.

Jedwali Na.1: Baadhi ya Istilahi Ngumu Zilizobainishwa na Watoataarifa

Na	Istilahi za Kiswahili	Istilahi za Kiingereza
1	Sasisha	Updates
2	Gotoka	Done
3	Nywira	Password
4	Pasiwaya	Wireless
5	Msimbo	Code
6	Sakinisha	Install
7	Kivnjali	Browser

Chanzo: Data za Uwandani (Julai 2021)

Katika Jedwali Na 1 tunaona baadhi ya istilahi zilizodaiwa kuwa ni ngumu, zilizobainishwa na watoataarifa. Mathalani istilahi *nywila*, *msimbo*, *gotoka na sakinisha* ni mionganini mwa istilahi zilizoonekana kuwa ngumu kwa watoataarifa kuzielewa. Utafiti ulibaini kuwa, watoataarifa wanaziona istilahi hizi kuwa ni ngeni na hawajawahi kuzisikia. Hivyo, wanaziona kwenye simu na wanashindwa kuelewa kuwa zinafumbata dhana gani kimatumizi. Utafiti unaonyesha kuwa, watoataarifa ambao ndio watumiaji, wanaona ni bora watumie istilahi za Kiingereza hata kama ni kwa kutohoa na kutafsiri wujuavyo, kuliko kutumia istilahi za Kiswahili ambazo hawazielewii. Katika sehemu inayofuata tunawasilisha Kielelezo Na.2. kinachoonyesha asilimia za waliota sababu hii.



Kielelezo Na.2: Istilahi za Kiswahili za Kitehama ni Ngumu


Katika Kielelezo Na.2 cha data tunaona kuwa watoataarifa 32 sawa na asilimia 50.70 ya watumiaji wa simu za mkononi hawatumii istilahi za Kiswahili za kitehama. Watoataarifa walibainisha kuwa istilahi zilizopo katika simu hazijazoleka mionganini mwao. Watoataarifa waliongeza kuwa maneno haya ni kana kwamba yamefyatuliwa kiwandani yakaletwa kwa wazungumzaji. Kwa sababu hiyo, wazungumzaji wanapata ugumu, wanapoteua Kiswahili, kutumiwa katika programu za simu. Aidha, Massamba (1997) anaeleza kwamba, mojawapo ya sababu za kutokubaliwa kwa istilahi za Kiswahili ni kuwa, watumiaji wanaona wanaistilahi wameunda maneno mapya ambayo ni magumu kwao. Massamba anatolea mfano wa watumiaji wanaosikika wakisema, ‘hawa wataalamu wa Kiswahili wanakifanya Kiswahili kuwa kigumu mno’. Anaendelea kueleza kwamba, hapa watumiaji wanamaanisha kuwa wanataka istilahi kuwekwa katika lugha ya kawaida waliyoizoea. Jambo hili linatoa taswira kuwa, kuna walakini katika suala la uundaji wa istilahi za Kiswahili za kitehama zinazotumika katika simu.

Madai ya watoataarifa kuwa baadhi ya istilahi za Kiswahili ni ngumu na hawazielewii si ya kupuuza. Hii ndiyo sababu, Kinyanjui (2014) anafafanua kwamba, istilahi zinapowekwa wazi kulingana na dhana, utata na mkanganyiko unawenza kuepukwa. Anaendelea kufafanua kuwa, istilahi zisipoleweka zitafanya mawasiliano yakatike na yakwame kati ya watumiaji. Kwa hiyo, kuna kila

sababu ya kufanya usanifishaji na usawazisho wa istilahi zilizoundwa kama ambavyo wataalamu wamewahi kushauri (taz. Mdee, 1999; Massamba, 2007; Kahigi, 2007; Kevogo, 2016). Usanifishaji na usawazisho utawezesha istilahi kueleweka na kuwa rahisi kwa watumiaji kuliko ilivyodhihirika katika makala haya. Ni dhahiri kwamba, istilahi za simu zilizoundwa na wataalamu ili zitumike, bado hazikidhi mahitaji ya watumiaji na wanaona ni maneno mageni kwao. Hali hii ya istilahi kuonekana ngumu kueleweka, inatoa picha kwamba, istilahi hizi si rafiki na kubalifu kwa wazungumzaji.

Uelewakaji wa Istilahi za Kiingereza Kwenye Simu

Watoataarifa 38 kati ya watoataarifa 62 walisema kuwa istilahi za Kiingereza zilizoko kwenye simu za mkononi zinaeleweka kwa urahisi zaidi kuliko Kiswahili. Jambo hili lilichochea haja ya kutaka kujua zaidi kwa nini watoataarifa waelewe istilahi za Kiingereza za kitehama za simu kuliko za Kiswahili? Watoataarifa waliongeza kuwa hali hii inatokana na jinsi simu zao zilivyokuja zikiwa na lugha ya Kiingereza na kuwafanya wajizoeze kuzitumia kuliko za Kiswahili zilizoundwa baadaye. Uwasilishaji wa asilimia umeonyeshwa katika kielelezo Na. 3.




Kielelezo Na.3: Istilahi za Kiingereza Kwenye Simu ni Rahisi

Katika Kielelezo Na 3 hapo juu, tunaona asilimia 60 ya watoataarifa walisema kwamba, istilahi za Kiingereza za kitehama ni rahisi kuliko Kiswahili. Watoataarifa walieleza kuwa, simu zilizo nyingi, zilizoanza kuingizwa nchini Tanzania na Afrika Mashariki, hazikuwekewa lugha ya Kiswahili badala yake ziliwekewa Kiingereza kama lugha chanzi. Kwa msingi huo, baadhi ya watumiaji wa simu walijizoesha kutumia istilahi za Kiingereza za simu kuliko Kiswahili. Utafiti ulibaini kuwa, mazoea ya kutumia istilahi za Kiingereza za simu, yamewafanya kuzoea istilahi za Kiingereza, japokuwa ni kwa kukariri ili kufanikisha mawasiliano yao. Kevogo (2016) anaeleza kuwa, mazoea ya kukariri istilahi za Kiingereza za kitehama yamewafanya watumiaji wa simu waanze kujiundia istilahi zao watakavyo, hata kama hazitambuliki katika mfumo rasimi, ingawa wanazitumia.

Kutumia Istilahi za Kiswahili za kitehama katika Simu ni Ushamba

Mtazamo hasi dhidi ya Kiswahili walionao baadhi ya wazungumzaji ulijidhihirisha katika utafiti huu. Watoataarifa 3 kati ya 62 ya watoataarifa walidai kuwa hawatumii istilahi za Kiswahili za simu kwa kuwa huo ni ushamba. Sababu hii ilikuwa ni ya kushangaza sana, kwa sababu watumiaji wa simu ambaa pia ni wazungumzaji wa Kiswahili wanajaribu kuikana lugha yao. Sababu hii ilikolezwa na madai kutoka kwa watoataarifa kwamba, ‘jamii ya Tanzania tumetawaliwa na ukoloni’ hivyo, tunajiona kuwa kutumia Kiswahili ni kujitweza. Hii inamaanisha kuwa, kutumia istilahi za kitehama za Kiswahili katika simu za mkononi, utaonekana uko nyuma na wala si wa kisasa. Kulingana na watoataarifa, lugha ya Kiingereza iliyokuja na simu za mkononi, ni ya maana kuliko lugha nyingine. Aidha, wanaona kuwa mtumiaji wa istilahi za kitehama za Kiingereza katika simu ndiye wa kisasa. Katika Kielelezo Na.4 tunawasilisha asilimia za waliota sababu hii.




Kielelezo Na.4: Kutumia Istilahi za Kiswahili za Simu ni Ushamba

Katika kielelezo Na 4 cha data hapo juu tunaona asilimia 5 ya watoataarifa walieleza kuwa kutumia istilahi za Kiswahili za simu ni ushamba. Utafiti umebaini kwamba, baadhi ya watumiaji wa simu wanaozungumza Kiswahili wanaikana lugha ya Kiswahili iliyobeba utamaduni na utu wao kwa ujumla. Akikosoa mtazamo kama huo, Qorro (2007) anaeleza kuwa, mtu kuikana lugha yake ni suala la kisaikolojia linalomfanya asijiamini na anakosa mahali pa kuanzia. Qorro anaendelea kufafanua kuwa, mtu huyo anayachukia mambo yake yote, yaani, anaushuku utu na ubinadamu wake. Anaongeza kwamba, mtu hajiamini kama amekamilika mpaka akamilishwe na vya wengine. Alisisitiza kwamba, ili mtu akamilike, anapaswa kujiamini na kujithamini ikiwa ni pamoja na kuthamini vya kwake ikiwemo lugha yake. Matokeo haya yanaonyesha kuwa baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu bado hawazipi istilahi za Kiswahili za kitehama nafasi ya kwanza katika simu zao.

Mtazamo hasi dhidi ya hali ya matumizi na kutozikubali istilahi za Kiswahili walionao wazungumzaji wa Kiswahili, umeenea kwingi mionganii mwa watu wa Afrika Mashariki. Kamau (2007) anabainisha kuwa wazungumzaji wengi wa Kiswahili wana mtazamo hasi dhidi ya lugha yao. Hii ndiyo maana wanapendelea kutumia istilahi za Kiingereza za kitehama katika teknolojia ya mawasiliano na miktadha rasmi. Kamau anaendelea kufafanua kwamba, jambo hili, linadhihirika zaidi katika nchi za Uganda na Kenya. Hata hivyo, utafiti wetu umeonyesha kuwa hata nchini Tanzania mtazamo hasi wa wazungumzaji dhidi ya kukutumia Kiswahili katika simu upo. Hali hii imejidhihirisha katika hoja kuwa, kutumia istilahi za Kiswahili katika programu za simu ni ushamba. Kwa msingi huo, tunawahimiza wazungumzaji wa Kiswahili, wanaotumia simu wawe wazalendo kwa lugha yao. Hivyo, tunasisitiza wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mkononi, kuiithamini lugha yao adhimu, kwa kuitumia katika kila nyanja inakotumika zikiwemo za mawasiliano katika simu za mkononi.

Kiingereza ni Lugha ya Kimataifa

Watoataarifa 2 kati ya watoataarifa 62 walisema kuwa wanatumia Kiingereza kwenye simu kwa sababu Kiingereza ni lugha ya kimataifa. Utafiti ulionyesha kwamba watoataarifa wanaichukulia lugha hii kama lugha inayotoka katika nchi zilizoheshimika na inatumia na watu wengi duniani. Waliongeza kuwa wanakipenda Kiingereza kwa kuwa ni lugha ya kibiashara. Watoataarifa walifafanua kwamba wanajinasibisha na umataifa wa lugha ya Kiingereza kama sababu ya kuipenda kuliko kutumia istilahi za Kiswahili katika programu za simu za mkononi. Uwasilishaji zaidi wa asilimia umeonyeshwa katika Kielelezo Na .5.



Kielelezo Na.5: Kiingereza ni Lugha ya Kimataifa


Katika kielelezo Na 5 hapo juu tunaona asilimia 3 ya watoataarifa walidai kuwa, wanatumia istilahi za Kiingereza za simu za mkononi, kwa sababu Kiingereza ni lugha ya kimataifa. Utafiti umebaini kuwa, watumiaji wa simu wanaozungumza Kiswahili, wanajaribu kujinasibisha na umaarufu wa lugha ya Kiingereza kama sababu ya kuipenda, kuliko kutumia istilahi za Kiswahili kitehama katika simu za mkononi. Aidha, ilibainika kuwa kuona kwamba Kiingereza ni lugha ya kimataifa, kunawafanya watumiaji wa simu wanaozungumza Kiswahili, wathamini sana Kiingereza kuliko lugha ya Kiswahili. Jambo hili, lina changamoto kubwa katika hatua ya ustawi na maendeleo ya jamii yetu. Hii ndiyo sababu, Senkoro (2007) anaeleza kwamba hakuna nchi hata moja duniani iliyopata kuendelea kwa kutumia lugha ya Kigeni. Anaendelea kufafanua kwamba, nchi zote tuonazo zikiinukia kimaendeleo leo hii, zimeendelea na zinazidi kuendelea kwa kutumia lugha zao kwa vile masuala yote muhimu yamo katika mawazo yanayoelezwa kikamilifu kwa lugha zao. Tunaungana na mawazo ya Senkoro kwa sababu mbili. Mosi, istilahi za kitehama za Kiswahili zimefumbata maana zitumiwazo na wazungumzaji wa Kiswahili. Pili, ni jambo la hatari kwa watumiaji wa simu wanaozungumza Kiswahili kujinasibisha na lugha ya Kiingereza kwa kuiona ya thamani na kudunisha matumizi ya istilahi za kitehama za Kiswahili. Kufanya hivyo ni sawa na kutweza Kiswahili. Utafiti umebaini kwamba, ni muhali kuyafikia maendeleo ya kweli yanayotokana na kuthamini na kutumia lugha nyingine isiyo na chembe ya utamaduni wetu. Katika hili, tunasisitiza kwamba maendeleo ya kweli katika nyanja zote za binadamu yatafikiwa ikiwa tutathamini na kutumia lugha yetu aushi na adhimu ya Kiswahili.

Sababu Nyinginezo

Mbali na sababu zilizotolewa na watoataarifa, ambazo tumezichukulia kama sababu za msingi zinazowafanya wazungumzaji wa Kiswahili kutotumia istilahi za kitehama za Kiswahili za simu, utafiti ulibaini kuwepo kwa sababu nyinginezo, ambazo zilionekana kuwa kikwazo kwa wazungumzaji kutotumia istilahi za Kiswahili za simu zao. Sababu hizo zimefanuliwa katika sehemu zinazofuata.

Mfumo wa Simu Hautoi Fursa ya Kuchagua Lugha Nyingine

Watoataarifa 29 kati ya 62 walisema kuwa, hawatumii istilahi za Kiswahili za kitehama kwenye simu, kwa kuwa, mfumo wa simu katika baadhi ya simu, umewekwa katika lugha ya Kiingereza na siyo lugha ya Kiswahili. Matokeo yalionyesha kwamba, mpangilio wa uteuzi wa lugha kwenye programu za simu, hautoi fursa kwa mtumiaji kubadilisha lugha moja kwenda nyingine. Isipokuwa kubaki katika lugha iliyokuja na simu. Uwasilishaji zaidi wa asilimia umeonyeshwa katika Kielelezo Na. 6.




Kielelezo Na.6: Mfumo wa Simu Hautoi Fursa ya Kuchagua Lugha Nyingine

Katika Kielelezo Na 6 cha data yetu hapo juu tunaona kuwa asilimia 46.03 ya watoa taarifa walidai kwamba mifumo ya baadhi ya simu haina vitufe elekezi vya kuchagulia lugha. Utafiti ulionyesha kuwa, vitufe hivyo, ni vile vinavyowawezesha watumiaji wa simu kuchagua lugha nyingine tofauti na lugha ya Kiingereza iliyokuja na simu. Matokeo yalionyesha kuwa, simu zenye changamoto hiyo ni za mifumo ya *android* na *apple* zinazofahamika kama simujanja (*smartphone*) kuliko simu zilizo katika mfumo wa analogia. Kwa mfano, katika utafiti wetu, ilibainika kuwa kati ya watumiaji 10 wenye simujanja ni watumiaji wawili au watatu ambao simu zao zinaweza kuruhusu kuteua lugha nyingine tofauti na Kiingereza.

Madai haya ya watoataarifa kuhusu simu kukosa vitufe vya kuchagulia lugha hususani ya Kiswahili, yanatoa sura mchanganyiko kwa watumiaji wa simu kutumia au kutotumia istilahi za Kiswahili za programu za simu. Hii inatokana na ukweli kwamba, mtumiaji wa simu, angetamani atumie istilahi za Kiswahili za kitehama katika simu, isipokuwa simu anayoitumia haina kitufe wezeshi cha kuteulia lugha nyingine. Kwa hiyo, mzungumzaji anayetumia simu atalazimika kutumia istilahi za lugha iliyokuja na simu, hususani Kiingereza. Utafiti ulionyesha kuwa, mkwamo huo unawakumba baadhi ya watumiaji wenye simu hizo ilhali walitamani kutumia istilahi za Kiswahili za programu za simu. Utafiti umebaini kwamba changamoto hii ya kiufundi inawakwaza baadhi ya watumiaji wa simu, wanaozungumza Kiswahili waliotamani kutumia istilahi za Kiswahili za programu za simu.

Kutofahamu Kubadilisha Simu Kwa Lugha ya Kiswahili

Utafiti umebaini kuwa, baadhi ya watumiaji wa simu, wanakabiliwa na changamoto ya ufahamu wa kutumia vifaa vya mawasiliano, hususani, simu za kisasa za mkononi maarufu kama simujanja. Watoataarifa 3 kati ya 62 walisema kuwa, hawafahamu kabisa kubadilisha simu, kutoka Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili. Watoataarifa walieleza kwamba, nyenzo za mawasiliano kama simu, ni bidhaa ambazo hazitengenezwi nchini Tanzania. Aidha, walionegeza kwamba, si rahisi kwa watumiaji wa mara ya kwanza kuwa na maarifa ya matumizi ya vifaa hii. Uwasilishaji zaidi wa asilimia umeonyeshwa katika Kielelezo Na 7.




Kielelezo Na.7: Watumiaji Hawafahamu Kubadili Lugha kwenda Kiswahili

Katika kielelezo Na 7 hapo juu tunaona asilimia 4.76 ya watoataarifa walitoa sababu kuwa hawafahamu kuchagua lugha nyingine kwenye simu. Utafiti ulionyesha kuwa, baadhi ya watumiaji hawana maarifa ya kutosha kuweza kuchagua lugha nyingine tofauti na ile waliyoikuta kwenye simu, hususani Kiingereza. Hali ya watumiaji kukosa maarifa ya kubadilisha lugha katika simu zao, inatokana na ukweli kuwa, nyenzo za mawasiliano kama simujanja za mkononi, ni vifaa vya kisasa, ambavyo watumiaji hawana uzoefu navyo. Kwa hiyo, kutokuwa na maarifa, ni mojawapo ya vikwazo vinavyowafanya watumiaji washindwe kuzitumia simu kwa uhuru, kwa kuwa wanakosa maarifa ya kuteua lugha wanayoilewa, hususani, Kiswahili.

Katika sehemu hii, ugumu wanaoupata watumiaji wa simu, unatokana na kutokuwa na maarifa ya kutumia simu za mkononi za kisasa, hususani simujanja. Kwa sababu hiyo, wanalazimika kutumia istilahi za lugha iliyokuja na simu, hususani Kiingereza. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, hawana ufahamu wa kuchagua lugha nyingine, hata kama kitufe cha kuchagua lugha hiyo, kipo.

Kutofahamu Kama Kuna Kiswahili Katika Simu Kuliko Kiingereza

Watoataarifa 2 kati ya 62 walisema kuwa, hawatumii istilahi za Kiswahili za simu, kwa sababu hawajui kama kuna lugha nyingine katika simu za mkononi tofauti na Kiingereza. Hii ina maana kuwa, ujio wa teknolojia ya mawasilaino na lugha zilizopo katika vifaa hivi haifahmiki kwa baadhi ya watumiaji wa simu hizo. Hiki ni miongoni mwa vikwazo vya utumiaji wa istilahi za Kiswahili za kitehama katika simu za mkononi. Uwasilishaji zaidi wa asilimia umeonyeshwa katika Kielelezo Na.8.



Kielelezo Na.8: Hawajui Kama Kuna Kiswahili kwenye Simu

Katika Kielelezo Na 8 cha data tunaona asilimia 3.17 ya watoaarifa walidai kuwa hawafahamu kama kuna lugha nyingine, mfano, Kiswahili kuliko Kiingereza katika simu. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, baadhi ya watumiaji wa simu hawana maarifa ya kutosha kuhusu utumiaji wa simu za mkononi. Utafiti umebaini kwamba kutokuwa na maarifa ya namna ya kuzitumia simu, kunawafanya wasijue kama kuna istilahi za kitehama za Kiswahili kwenye simu.

Utafiti umebaini kwamba, vikwazo vinavyowafanya baadhi ya wazungumzaji washindwe kutumia istilahi za Kiswahili, hazitokani na masuala ya changamoto za uundaji wa istilahi peke yake. Hii ni kwa sababu, utafiti umeonyesha kuwa, kuna sababu mbalimbali zinazowafanya wazungumzaji wasitumie istilahi za Kiswahili. Sababu ya kwanza ni mifumo migumu ya kiteknolojia iliyopo katika mipangilio ya simu za mkononi. Pili, ufahamu duni walionao baadhi ya wazungumzaji kuhusu kutumia simu za kisasa. Sababu hizi mbili zinachangia kuwafanya wazungumzaji washindwe kutumia istilahi za Kiswahili za kitehama za simu za mkononi.

Tathmini ya Matumizi na Kukubalika kwa Istilahi za Kitehama

Matokeo ya utafiti yamebainisha masuala mbalimbali ambayo ni muhimu kuyachambua na kuyajadili katika sehemu hii. Masuala yaliyoibuliwa na watoaarifa ni mtambuka kiasi kwamba hayawezi kuelezwu kwa namna moja peke yake. Masuala hayo ni pamoja na sababu zinazowafanya wazungumzaji watumie istilahi za Kiswahili za kitehama kwenye simu. Pia, sababu zinzowafanya wasitumie istilahi za Kiswahili, sababu nyinginezo zinazowafanya wazungumzaji washindwe kutumia istilahi za Kiswahili.

Utafiti ulionyesha kwamba, kundi la kwanza la wazungumzaji wa Kiswahili wanakubali kukitumia Kiswahili, kwa kuwa ni lugha mama. Pamoja na kuwa na sababu mchanganyiko watumiaji wa kundi hili walionyesha kuithamini lugha ya Kiswahili na kuonyesha mapenzi na uzalendo katika lugha hiyo. Baadhi ya watumiaji walionyesha masikitiko yao, hususani, wanapotumia simu zisizokuwa na mifumo rafiki ya uteuzi wa lugha. Hali hii huwafanya washindwe kuchagua lugha ya Kiswahili isipokuwa Kiingereza kilichokuja na simu. Kwa maoni yetu, Kiswahili kinapewa nafasi kiasi na baadhi ya wazungumzaji watumiao simu kutokana na changamoto wanazokabiliana nazo. Utafiti ulibaini kuwa, wazungumzaji wanakwama mara kwa mara kutumia simu hususani simujanja. Kukwama huko, kunatokana na vifaa hivyo, kutokuwa na vitufe hai vya uchaguzi wa lugha nyingine tofauti na Kiingereza. Aidha, ilibainika kwamba, istilahi za Kiswahili zilizowekwa katika vifaa hivyo zinaonekana kuwa ngumu kwa baadhi ya wazungumzaji. Utafiti ulidhihirisha kwamba, hali hiyo huwakatisha tamaa wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu na kuwavunja moyo, wanaopenda kutumia istilahi za Kiswahili. Mawazo kama haya, yaliwahi kudokezwa pia na King'ei (1999) akibainisha kwamba, maendeleo ya istilahi za Kiswahili yasiyoratibiwa, yameibua changamoto kadhaa zikiwemo; usawa usiotoshelevu wa istilahi, istilahi shindani za Kiswahili, istilahi potofu. kwa kutaja chache. Hali hii inatokana na ukosefu wa usanifishaji na usawazisho wa istilahi. tunashauri kuwa juhudzi za pamoja zichukuliwe katika kuunda istilahi za Kiswahili za programu tumizi za vifaa vya kiteknolojia zikiwemo simu za mkononi, printa, nukushi, mashine za kutolea fedha (ATM) na kompyuta. Vilevile tunashauri kwamba, juhudzi za pamoja kuchukuliwa na vyombo vyenye mamlaka na lugha ya Kiswahili nchini Tanzania ili kurekebisha hali hii. Hii ni kwa sababu, mahitaji ya matumizi ya vifaa vya kisasa vya mawasiliano kama simu za mkononi yanazidi kuongezeka kila uchao. Aidha, uvumbuzi wa vifaa vya kiteknolojia unazidi kuongezeka, kukua na kupata watumiaji. Ni matarajio yetu kwamba wanaistilahi washirikiane pamoja na wataalamu wa vifaa hivi vya teknolojia ili kuandaa istilahi za kitehama za Kiswahili zitakazotumika kwa namna moja mionganoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili.

Utafiti ulionyesha kwamba, kundi la pili katika utafiti wetu ni wazungumzaji wasiotumia istilahi za Kiswahili za simu za mkononi. Utafiti ulibaini kwamba, sababu za kundi hili zilidhihirisha kutothamini Kiswahili na utamaduni wake kwa watumiaji na kushindwa kuwa wazalendo kwa lugha yao. Kwa maoni yetu, wazungumzaji Kiswahili, wameamua kukitupilia mbali Kiswahili kwa kuwa wamekuwa watumwa ndani ya nchi yao wenyewe. Utafiti ulidhihirisha kwamba, wazungumzaji katika kundi hili, wamejinasibisha na lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili, kwa kukipa Kiingereza thamani na umuhimu mkubwa. Jambo hili la kutothamini vya kwetu ikiwamo lugha yetu ni sawa na

kujikataa wenyewe. Kwa maoni yetu, pamoja na ukweli kuwa kila mtu ana utashi wake wa kutumia lugha vile anavyoridhika, bado madai haya ya watoataarifa hayawezi kupita bila kusailika. Mathalani, kwa maoni yetu ni jambo linalosailika kuona kwamba, kutumia istilahi za Kiswahili kwenye simu ni ushamba. Hii ni kwa sababu, unapodharau lugha yako na kutukuza vya wengine si tu kuwa wewe ni mtumwa wa lugha hiyo, bali pia, unakuwa umetekwa kifikra. Tunaona kuwa, mitazamo kama hii, ni matokeo ya kasumba za baadhi wazungumaji wa Kiswahili ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitokuza sana Kiingereza kuliko Kiswahili japokuwa wanazungumza Kiswahili kila siku.

Utafiti ulibaini kuwa, madhara ya ukoloni mamboleo na mifumo iliyowakuza baadhi ya wanajamii wengi, kudhani kuwa, kujua kuongea Kiingereza ndio usomi au ndio kilele cha maarifa ni mtazamo ambao sio tu kwamba unasailika bali pia ni hasi. Pia, utafiti ulibaini kwamba kama jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili, tumekuwa na hali ya kusitasita kwa muda mrefu kutohana na utashi wa baadhi ya watangulizi waliokuwa wakibeza matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili. Vilevile, utafiti ulionyesha kwamba, kwa sasa imedhihirika kwamba Kiswahili kinajitosheleza kuwa lugha ya mawasiliano mapana duniani. Kwa mfano; juhudini zilizofanywa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na wataalamu wake wa Kiswahili pamoja na wapenzi wa Kiswahili duniani kote zimefanya lugha ya Kiswahili kutambuliwa kimataifa. Aidha, uamuza wa kuwa na siku maalumu ya Kiswahili kila tarehe saba, Julai ya kila mwaka, uliotangazwa na shirika la maendeleo ya sayansi, elimu na utamaduni duniani (UNESCO), ni wa kupigiwa mfano. Siku hii imeanza kusherekewa Tanzania na katika mataifa mbalimbali ya Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla kuanzia Julai saba mwaka 2022. Hii inaonyesha kuwa, Kiswahili sasa kimepea na kushika kasi kama moto wa nyika katika anga za kimataifa. Wanaokiona na kukiweza kwa kufikiri kuwa ni Kiingereza pekee ndio lugha ya kimataifa wana jambo la kujifunza kupitia Kiswahili.

Aidha, tuna maoni kwamba, taasisi zinazosimamia Kiswahili mathalani, BAKITA TATAKI na BAKIZA, zipitie upya sera zilizopo kuhusu lugha ya Kiswahili na utangamano wa kimataifa katika masuala ya biashara za kimataifa. Lengo la kuzipitia upya sera za lugha zilizopo, ni kupata sera bora na jumuishi itakayofumbata matakwa na mahitaji ya bidhaa zinazoletwa nchini, kuwekewa lugha ya Kiswahili. Jambo hili likifanikiwa litaiwezesha lugha kutumiwa kupitia bidhaa hizo. Kwa mfano, kuwepo kwa sera kunawezesha kutungwa kwa kanuni au sheria. Kanuni hizi, zitatumika kuwaelekeza watengenezaji wa bidhaa kama vile, simu za mkononi na kuziwekea lugha ya Kiswahili, hususani kwa simu zinazokuja Tanzania na Afrika Mashariki ambamo Kiswahili kinazungumzwa.

Hitimisho

Makala haya, yameonyesha kuwa hali ya matumizi ya istilahi za Kitehama za Kiswahili za simu kwa watumiaji wanaozungumza Kiswahili imeghubikwa na mitazamo mchanganyiko. Makala yameonyesha kuwa, wazungumzaji wa Kiswahili wana sababu mbalimbali zinazowafanya watumie au wasitumie istilahi za kitehama za Kiswahili za simu. Vilevile, makala imebainika kuwa, urahisi wa Kiswahili na kutumiwa kwa muda mrefu lugha hii kama lugha ya mawasiliano katika jamii, ni mingoni mwa sababu zinazofanya baadhi ya watumiaji wa simu wakubali kutumia istilahi za Kiswahili za kitehama za simu. Kwa upande mwingine, Makala yameonyesha kuwa baadhi ya istilahi za Kiswahili za programu za simu zilizoundwa kutumiwa katika programu za simu ni ngumu na hazieleweki kwa watumiaji wa simu, wanaozungumza Kiswahili. Jambo hili, linawachagiza wanaistilahi na wataalamu wa lugha kuzitathmini mbinu za uundaji wa istilahi za kitehama ili kupata istilahi rafiki, na zinazoeleweka kwa namna moja mionganoni mwa watumiaji wa simu za mkononi.

Katika makala haya, tumebaini kuwa changamoto za ugumu wa istilahi za Kiswahili za Kitehama za simu, zinapaswa kukabiliwa kwa kuwashirikisha, watumiaji wa simu za mkononi. Tuna maoni kwamba, si jambo jema, waundaji wa istilahi kujifungia peke yao katika majopo ya uundaji wa istilahi. Tuna maoni kwamba, kuwatenga watumiaji wa istilahi katika mchakato wa uundaji wa istilahi ni sawa na kuandaa chakula (istilahi za Kiswahili za kitehama za simu za mkononi) kisichokuwa na walaji (wazungumzaji wa Kiswahili wanaolengwa kuzitumia istilahi za simu zinazoundwa). Makala haya, yanachokoza na kuchagiza vyombo vilivyopewa dhamana ya kusimamia Kiswahili nchini Tanzania, mathalani, BAKITA na BAKIZA, wataalamu na waundaji wa istilahi, kuzipitia upya

istilahi za simu za mkononi ili kufanya usawazisho. Zoezi la usawazisho litaondoa upungufu wa istilahi za kitehama zilizoundwa. Tunapendekeza kwamba, zoezi la upitiasi upya istilahi, liwashirikishe wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mkononi. Mohochi (2007) anaeleza kwamba, baadhi ya wataalamu wanakubali istilahi za Kiswahili zina upungufu kwani bila kukubali kuwepo kwa tatizo si rahisi kulitafutia utatuvi. Ni maoni yetu kuwa, matumizi ya istilahi za Kiswahili za kitehama za simu za mkononi yataongezeka ikiwa hatua madhubuti zitachukuliwa na wadau wote wa Kiswahili.

Marejeleo

- Ferber, H. (1980). "International Standardization of Terminology: Theoretical and Methodological Aspects", katika *International Journal of the Sociology of Language*, De
- Kahigi K.K (2007). Ujanibishaji wa office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu. Katika Senkoro F.E.M.K na Kahigi K.K (Wahariri) *Kiyo Cha Lugha*. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuuy ya 5.
- Kamau S. N (2007). A Digital Africa Kiswahili Holds the Key katika *African Journal Online* <https://www.ajolif/index.php/article/view/41764>
- Kevogo, S.A (2016). "Ukuzaaji wa Istilahi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano: Mifano wa Jitihada zisizo Rasmi za Kampuni na Watumiaji wa Simu za Mkononi Nchini Tanzania" Katika Mwita L.C (Mh.) *Kiswahili na Utandawazi*.Twaweza Communications Ltd. Nairobi Kenya.
- Kihore, Y.M. (2000). "Makala za kuchoea utafiti wa Kiswahili na Teknolojia ya Habari", katika *Mulika* Na. 26.TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimijamii*. TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kinyanjui, J.M. (2014). Challenge of Competing Neologisms: A case of Kiswahili Technical Terminology. Nairobi: University of Nairobi (Tainifu haijachapishwa)
- LOT (2009). *Atlas ya Lugha za Tanzania*: Mradi wa Lugha za Tanzania Inforbridge Consultants Dar es Salaam.
- Malangwa, P. S. (2010). Handling Technical Translations: The Case of Translations of Computer
- Massamba D.P.B (1997). "Problems of Terminology Development: The Case Study of Tanzania, katika *Kiswahili* Dar es Salaam TUKI. Juzuuy ya 59. Kur.86-98.
- Mdee, J.S (1999). "Matumizi ya Istilahi katika Kiswahili na Jinsi Yanavyoathiri Kiswahili," MULIKA Na. 25, Dar es Salaam:TUKI.
- Mgullu, R.S (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohochi, S. (2007). "Jungu Kuu Limeisha Ukoko? Uendelezaji wa Kiswahili Kupitia Uundaji wa Msamiati", katika Senkoro (Mhariri) *Lugha na Fasibi ya Kiswahili Afrika Mashariki*: Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki.
- Nida, E. A. na Taber, C.R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E. J. Brill.
- Okyere S. M, Oduori, W.R. na Magugu, V.N (2016). "Ubinafsishaji wa Dhana Kupitia Tafsiri: Uchanganuzi wa Lugha katika Rununu ya Nokia", katika Jilala H (Mhariri) *Nadbaria za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi* Dares salaam: Daud Publishing Company Limited.
- Qorro(2007)."Matatizo ya Kufundisha kwa lugha za kigeni katika nchi za Afrika: Kwa Mfano, Kiingereza katika shule za sekondari Tanzania", katika Senkoro F.E.M.K (Mhariri) *Lugha na Fasibi ya Kiswahili Afrika Mashariki*:Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki.
- Sager, J.C. na Johnson, R.L. (1978). "Terminology:The State of the State of the Art", katika *Der Sparachmittler*. AILA Bulletin 22.
- Sanday, W.A (2014). Evaluating the Acceptance and Usability of Kiswahili localized Mobile Phone App in Kenya: A case of M-Pesa App. Nairobi University of Nairobi (Tasinifu Haijachapishwa).
- Senkoro. F.E.M.K (2007)."Mauaji ya Halaiki ya Watoto wa Tanzania Kupitia katika Lugha ya Kufundishia Sekondari na Vyuooni",katika Senkoro (Mhariri)*Lugha na Fasibi ya Kiswahili Afrika Mashariki*:Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki.
- Tumbo-Masabo, Z.N.Z na Mwansoko, H.J.M (2008).*Kiongozi Cha Uundaiji wa Istilahi za Kiswahili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.
- Yambi, J. (1988). "Uundaiji wa Istilahi za Kiswahili na Usambazaji wake" katika *KISWAHILI*. TUKI. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam: Juz.55/1 & 55/2, uk. 152-162.

